

**FAIDA>> Mfumo wa c**

## TALIRI yaanika mkakati mpya kuboresha uchumi kwa wafugaji

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), imesema imejipanga kuinua uchumi wa wafugaji kwa kuwapa mbinu madhubuti ya ufugaji wa kisasa.

Akizungumza jana katika maonyesho hayo, Mtafiti wa Mifugo, Valentino Urasa alisema taasisi ina vituo saba ambavyo vimegawanywa katika kanda za utafiti ikiwemo Makao Makuu Tanga.

TALIRI ina vituo vinne katika mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam.

Urasa alisema lengo la taasisi ni kuona wafugaji wana mifugo bora na yenye kuleta tija katika kukuza uchumi.

Alisema taasisi inatumia teknolojia ya ng'ombe wa maziwa amba wanastahimili hali ya hewa ya mkoani Pwani.

"Taasisi yetu inatoa huduma ya ufugaji katika mikoa ya Pwani na hata ng'ombe wanaofugwa katika maeneo hayo wanastahimili hali ya hewa," alisema.



**Teknolojia hiyo ya malisho  
bora kwa mifugo yetu  
tunaisambaza kwa wafugaji ili  
kila mfugaji aweze kufaidika  
na teknolojia hiyo.**

Mtafiti wa Mifugo,  
Valentino Urasa

Aliongeza kuwa ng'ombe wanaofugwa katika mikoa hiyo wanapatiwa malisho bora ili watoe maziwa kwa wingi.

"Teknolojia hiyo ya malisho bora kwa mifugo yetu tunaisambaza kwa wafugaji ili kila mfugaji aweze kufaidika na teknolojia hiyo", alisema.

Alisema jani la jumkao limekuwa mkombozi kwa wafugaji wengi.

Alisema wapo katika maonyesho hayo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafugaji na kutoa teknolojia walizonazo.

Mtafiti kutoka TALIRI, Walter Mongesho, alisema lengo la kufika katika maonyesho hayo kuona kama teknolojia zao zimeleta tija kwa wafungaji.

"Tumekuja katika maonyesho haya ili kuona kama teknolojia tunazosambaza zinaleta tija kwa wafungaji wetu," alisema.

Mongesho alisema kutohana na tafiti zinazofanywa na TALIRI idadi ya vifo vy ya nyama imepungua kutohana na teknolojia ya malisho iliyopo.

## Maboresho Feri kuanza Julai hii



**Dar es Salaam.** Baada ya zabuni ya kumpata mkandarasi kutangazwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvu imesema ukarabati wa Soko la Samaki Feri jijini hapa utaanza mwezi huu.

Katika maandalizi ya awali, Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Mashimba Ndaki akiambatana na nailbu wake, Abdallah Ulega walizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo kujiaandaa na ukarabati huo huku akiwahakikishia kuwa hakuna atakayeo-ndolewa.

"Niwatoe hofu hakuna atakayeo-ndolewa. Tutawahamisha kwa muda kupisha ukarabati. Ukikamilika mtare-jea, tunatarajia kuanza kanda namba moja na mbili ambazo zina changamoto," alisema Ndaki.

Akizungumzia siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, Ndaki anasema kuna maboresho mengi ya miundombinu yamefanyika kwenye sekta ya uvuvu baharini hata kwenye maziwa makuu. Hivi sasa, anasema ujenzi wa mialo sita unaendelea Ziwa Victoria, Soko la Samaki Mbamba Bay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma na Sh50 bilioni zimetengwa kujenga Bandari ya Uvuvu Mbegani, Bagamoyo.

"Serikali imenunua boti 12 na injini sita za kupachika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvu na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvu imetoka taarifa kwa wavuvi 100 wa Bahari ya Hindi kuhusu maeneo yenye samaki," amesema Ndaki.

Ili kuongeza upatikanaji wa samaki, waziri anasema Serikali imetenga Sh18 bilioni zitakazotumika kupanua miundombinu ya vituo sita vya kuendeleza ukuzaji vlumbemaji vya Mwamapuli (Tabora), Ruhila (Ruvuma), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi), Machul (Tanga), na Rubambagwe mkoani Geita.



Pia amesema Serikali inahamasisha kilimo cha mwani katika maeneo ya Mkinga (Tanga) na Mchinga (Lindi) na wfugaji wa majongoo bahari wa Bagamoyo wamenunuliwa vitendea kazi vya Sh15 milioni.

"Juni 22 mwaka huu, kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Kusimamia Uvuvu wa Bahari Kuu (DSFA) ilikusanya Sh1.84 bilioni za malipo ya leseni za uvuvu kutoka meli 22. Meli za kigeni zilisitisha kuchukua leseni Tanzania tangu mwaka 2017/18, hivyo Serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kuijendesha," amesema.

Upande wa mifugo, Ndaki amesema "Serikali imechimba visima virefu viwili mkoani Iringa, imekarabati mabwawa matatu ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro) na kutenga hekta 32,044.21 wilayani Tanganyika, Nsimbo na Mlele kwa ajili ya malishi."

Kuhakikisha mnyororo wa thamani unakuu na tija zaldi, amesema wachuna ngozi 340 wa machinjio za Kinondoni na Temeke wamepewa mafunzo kupata ngozi bora. (Bakari Klang'o)